

*Yesu kwetu ni rafiki, hwambiwa haja pia; tukiomba kwa Babaye, maombi asikiya. Lakini twajikosesho, twajitweka vibaya; kwamba tulimwomba Mungu, dua angesikia.*

*Una dhiki na maonjo? Una mashaka pia. Haifai kufa moyo, dua atasikia. Hakuna mwingine mwema, wa kutuhurumia; atujua tu dhaifu; maombi asikia.*

*Je hunayo hata nguvu, huwezi kwendelea, ujapodharauliwa, ujaporushwa pia. Watu wangekudharau, wapendao dunia, hukwambata mikononi, dua atasikia.*

---

Je! unajua historia ya wimbo huu?

Joseph Scriven alizaliwa mnamo 1819 katika familia ya kitajiri huko Banbridge, County Down, Ireland. Alihitimu digrii yake kutoka Chuo cha Trinity, huko Dublin mnamo 1842. Mpenzi wake alizama kwenye maji na kufa kwa bahati mbaya mnamo 1843, usiku kabla ya kuolewa.

Mnamo 1845, akiwa na umri wa miaka 25, aliondoka nchi yake ya asili na kuhamia Canada, na kukaa Woodwood, Ontario. Alibaki Canada kwa muda

mfupi tu baada ya kuugua, lakini akarudi mnamo 1847

Mnamo 1855, alipokaa na James Sackville huko Bewdley, Ontario, kaskazini mwa Port Hope, alipokea habari kutoka kwa Ireland ya mama yake kuwa mgonjwa sana. Aliandika shairi la kumfariji mama yake inayoitwa “omba bila Kukata tamaa”. Baadaye iliwekwa kwa muziki na ikabadilishwa jina na Charles Crozat Converse, ikawa wimbo wa “Yesu kwetu ni Rafiki”. Scriven hakuwa na dhamira yoyote wala ndoto kwamba shairi lake litakuja kuchapishwa kwenye gazeti na baadaye kuwa wimbo unaopendwa kati ya mamilioni ya Wakristo ulimwenguni.

Ni nini tunaweza kujifunza kwa Joseph Scriven? Faraja kidogo kwa mama yake imekuwa faraja kwa mamilioni ya watu ulimwenguni...Lolote ufanyalo! au Kidogo umfanyiacho mtu aliye mnyonge, na aliye katika mashaka kinawenza Mungu anaweza kukifanya kuwa msaada kwa mamilioni ya wanyonge wengine mahali pengine.

---

### **Mada Nyinginezo:**

**JE! KUBET NI DHAMBI?**

**NAMNA YA KUITAMBUA SAUTI YA MUNGU INAPOZUNGUMZA NA  
WEWE**

## **JE! KUFANYA MASTURBATION (PUNYETO) NI DHAMBI?**

---

**Rudi Nyumbani:**

Share on:

WhatsApp